

Jina..... Nambari yako...../.....

Shule..... Tarehe

Sahihi yako.....

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

JUNI / AGOSTI / 2012

MUDA: SAA 2 ½

MTHANI WA TATHMINI WA PAMOJA YA SHULE ZA WILAYA YA BURETI- 2012

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

1. Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.
2. Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
3. Jibu maswali yote.
4. Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.

Kwa matumizi ya mtihani pekee.

swali	upeo	alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kfungu hiki kisha ujibu maswali.

Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) barani Afrika. Lugha ambazo zimekuwa zikitumiwa ni za kimagharibi kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kiingereza. Idadi kubwa ya Waafrika, hasa wanaoishi vijijini, hawazifahamu lugha hizi.

Uamuzi wa Shirika la Microsoft wa kutumia lugha ya Kiswahili katika programu za kompyuta kuanzia mwaka 2005 ni mchango mkubwa. Kuzinduliwa kwa mradi huu ni tukio la kipekee kuimarisha teknolojia sehemu za mashambani. Mradi huu umewawezesha wananchi takribani milioni 150 wa janibu za Afrika Mashariki kufaidi huduma za tarakilishi.

Utekelezaji wa mradi huu halikuwa jambo jepesi. Kwanza, ilibidi Shirika la Microsoft chini ya uongozi wa Bill Gates kulishawishi Bodi lake la wakurugenzi. Bodi liliposhawishika kuwa Kiswahili ni lugha inayotumiwa na mamilioni ya watu liliidhinisha kuzinduliwa kwa mradi. Hatua iliyofuatia ilikuwa kuteua maneno 700,000 ya kimsingi ya Kiingereza ambayo yangetafsiriwa kwa Kiswahili.

Hatua iliyofuata ilikuwa ushirikiano na dola pamoja na mashirika ya kibiashara na taasisi za kielimu ulimwenguni. Ilipobainika kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yangehamasisha uwekezaji katika vituo vya mtandao vijijini, ushirikiano katika kuendesha mradi huu uliafikiwa bila shida. Mradi huu ulichukua muda wa miezi 18 kukamilika. Uliwashirikisha wahusika katika uwanja wa teknolojia ya habari, mawasiliano, elimu, biashara na idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Vyuo vikuu hivi ni pamoja na Dar es Salaam, Nairobi, Kenyatta na Makerere,

Wataalamu walioshirikishwa walisaidia katika kubuni faharasa ya istilahi za Kiswahili 3,000. Hizi ni zile ambazo zinafaa kwa matumizi ya kompyuta ya kawaida na ya kila siku. Mradi huu umeshangiliwa na **wakereketwa** na wapenzi wa Kiswahili katika nyanja zote. Wasomi, wanariadha, wanamuziki, watalii, wafanyabiashara, wanasiya, wafuasi wa dini mbali mbali na wakulima; wote wamefurahia hatua ya Kiswahili kuingizwa kwenye mtandao.

Watu ambao walikuwa hawawezi **kuturisha** tarakilishi kwa sababu ya kutojua Kiingereza sasa hawana kisingizio. Matumizi ya Kiswahili yatapanua na kuimarisha mawasiliano baina ya watu wanaoishi vijijini na pembe zote za ulimwengu.

Jambo la kutia moyo zaidi ni kuwa sasa vyuo vikuu vinavyotoa masomo kwa kutumia mitandao vimepewa idhini ya kutumia programu hizi. Walimu na wanafunzi wanapata habari moja kwa moja kwa

Kiswahili bila kutafsiri. Kuna uwezekano sasa wa kusambaza mafunzo katika nyanja na viwango vyote kwa mfumo wa elimu ya mbali.

Katika ulimwengu wa utandawazi, tukio kama hili lina manufaa makubwa. Wananchi wa vijijini wanaweza kupata habari na maarifa kutoka pembe zote za dunia na kuhusu masuala tofauti tofauti kwa lugha wanayoielewa barabara.

Kusambaa kwa matumizi ya **ngamizi** vijijini kutaimarisha biashara inayofungamana na teknolojia ya mawasiliano. Hali hii itainua maendeleo ya kiteknolojia na kiwango cha maisha vijijini. Bila shaka mwachano uliopo baina ya sehemu za mijini na vijijini utapungua.

Haya ndiyo maendeleo anayokamia kila mja wa siku hizi. Lililopo ni serikali kupania kupanua na kusambaza muundo mbinu kama umeme na simu katika sehemu zote za nchi. Pamoja na haya, kuna haja ya kupunguza bei ya ngamizi na vipuri vyake ili kuwatia motisha watu kununua kompyuta kwa wingi.

Ikumbukwe kuwa lengo la kuanzisha mradi huu lilikuwa kuisaidia serikali kupanua na kusambaza matumizi ya huduma za kompyuta na mtandao katika shule, vituo vya kijamii na maeneo ya makaazi. Huduma hizi ni msingi wa elimu, biashara na mawasiliano ya kisasa.

Maswali

- (a) Eleza hatua zozote **nne** zilizotekelezwa ili kuingiza Kiswahili katika mtandao. (ala.4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- (b) Lugha imekuwa kikwazo kikubwa katika kukuza teknolojia ya habari na mawasiliano barani Afrika. Thibitisha kauli hii. (ala.2)

.....

.....

.....

.....

.....

(c) Taja faida **tatu** za mradi wa kutumia Kiswahili katika ratiba ya tarakilishi. (ala.3)

.....

.....

.....

.....

(d) Serikali inahitaji kufanya nini zaidi ili kufanikisha mradi huu? (ala.3)

.....

.....

.....

.....

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (ala.3)

i) Wakereketwa

.....

ii) Kuturisha

.....

iii) Ngamizi

.....

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Katika karne hii na ya kesho, urafiki ni ngome kuu duniani ambayo huhifadhi maslahi ya kila rafiki. Rafiki mwema humpenda mwenzake si kwa sababu ni tajiri ama ana cheo kikuu nchini. Rafiki mwadilifu huridhika na hali alyonayo rafikiye ; akiwa ni tajiri au ni masikini, ana cheo, hana. Rafiki mwema huwa mwadilifu wakati wowote. Wakati wa neema hushirikiana na rafikiye katika furaha na wakati wa shida hushirikiana naye katika huzuni na taabu zote zinazomkabili.

Sahibu mwema hutoa alichonacho kumkomboa rafiki yake, huwa radhi kabisa kufilisika kwa ajili yake. Mahali pa finyo hujasiri kuingia ili kumkomboa rafikiye, hushughulika zaidi kuliko wana ndugu wa toka nitoke. Kwa vyovyote hula naye tamu na chungu pamoja, mkono kwa mkono katika maisha yao yote hadi mmoja wao akaitoka dunia. Urafiki wa namna hii ndio uleto baraka ya Mungu, kuwashukia viumbe hao kama umande wa asubuhi.

Urafiki ni lazima sana katika maisha ya wanadamu. Urafiki ni mfano wa mishipa ipitishayo damu mwilini ili kurutubisha kila sehemu ya mwili. Ingawa ni bora kuwa na marafiki wengi lakini kila marafiki wanapozidi, ni hatari ya kuangukia kwenye marafiki wadanganyifu-hasidi. Pasi na shaka, ni heri maadui kuliko marafiki wadanganyifu. Hivyo basi, tukiwa na rafiki walio kinyume cha wema na upole wa kulinda haki za wanadamu na wasiomcha Mungu ni lazima tuwaepuke. Ingawa ni hivyo, vile vile sheria inatukataza tasisikilize na kujali ubaya wa mtu yeyote pasipo kuhakikisha. Huenda ikawa ni uvumi tu usiokuwa na msingi wowote. Ikiwa rafiki ni mbaya, hakosi atajulikana kwani mtungi mbovu haukawii kuvunjika. Lazima tuwapende watu wote ili kutimiza haki za kibinadamu na kuchukua matendo maovu. Rafiki waovu si vema kuwaacha katika maangamizi ya ubaya wao bali ni lazima tuwaambie waziwazi ili wapate kuongoka. Ukimsamehe rafiki, unaponya donda lake moyoni. Hivyo ni bora kuliko kumtazama na hali anazidi kukosa.

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Akifisha sentensi ifuatayo;

Rashid mama ulinipata wapi monika nilikuzaa mwanangu. (ala.2)

(b) Tumia neno '**kimya**' katika sentensi kama:

(i) kielezi (ala.1)

(ii) kihisishi (ala.1)

(c) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi;

Mtoto alisema kuwa angewatembelea kwao mwezi ambao ungefuata. (ala.3)

(d) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo

Gari la Juma limeibwa

Gari la Juma limeibiwa

(ala.2)

.....
.....
(e) Onyesha namna mbili za kuandika kitenzi ‘**cheza**’ katika hali ya kuamuru. (ala.2)

.....
.....
.....
.....
(f) Kwa kutumia mifano katika sentensi, onyesha matumizi **mawili mawili** ya alama hizi za uakifishaji.

(i) Dukuduku (ala.2)

.....
.....
.....
.....
(ii) Parandesi (ala.2)

.....
.....
(g) Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi — **ingine**.

i) Dau (ala.1)

.....
.....
(ii) Urembo (ala.1)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika **mazoea**.

Ua linalomea vizuri linietiwa rnbolea. (ala.1)

.....
.....

(i) Tunga sentensi kutofautisha jozi hizi kimaana. (ala1)

(i) Kua

.....
.....

ii) Kuwa (ala.1)

.....
.....

(j) Taja sauti zozote nne zinazotamkiwa katika **ufizi**. (ala.2)

.....
.....

(k) Kwa kutolea mifano taja a aina za **mofimu**. (ala.2)

.....
.....

(l) Watoto au vizalia wa viumbe hawa huitwaje. (ala.2)

(i) Paka

.....
.....

(ii) Nzige

.....
.....

(m) Bainisha aina za nomino zilizo tumika katika sentensi ifuatayo;

Kucheza kwa mwanafunzi kulimpendeza Mwalimu Juma. (ala.3)

.....
.....
.....
.....

(n) Eleza matumizi ya “KU” katika sentensi hii.

Kucheza huku hakufai (ala.2)

.....
.....

(o) Andika kwa udogo

(ala.2)

Ndege huyu alimla kifaranga

.....
.....

(p) Onyesha **kishazi huru** na **tegemezi** katika sentensi hii

Ijapokuwa kulikuwa na baridi kali niliondoka kwenda sokoni. (ala.2)

.....
.....

(q) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia **matawi**.

Mwanafunzi hodari anayechezea shule ya Hekima amepewa zawadi. (ala.4)

(r) Weka shadda panapofaa ili kubainisha maana tofauti ya neno ‘**walakini**’ (ala.1)

.....
.....

4. **ISIMU JAMU**

“Nakwambia adugu msikilizaji hapa mambo yamechacha kwelikweli. Hawa wachezaji wa Manyuu hawacheki na watu leo. Wameamua kuishambulia timu ya cheusi bila huruma. Kumbuka kwamba hii ni mara yao ya... Lo! Anauchukua mpira pale, mchezaji nambari tisa... Matiksta. Matiksta, Matiksta.....”

(a) Taja sajili inayorejelewa na dondoo ulilosoma (ala.2)

.....
.....
.....

(b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa **nne** zinazohusishwa na sajili uliyotaja hapo juu. (ala.4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

(c) Taja mambo **manne** yanayopelekea kufifia/kufa kwa lugha. (ala.4)

.....
.....
.....
.....